JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA



MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO WA RASILIMALIWATU KATIKA TAASISI ZA UMMA

CHANGANUA HAPA
KUSOMA MTANDAONI

YALIYOMO

DIBAJI iv
FARAHASA v

SURA YA KWANZA 1
DHANA YA MWONGOZO WA MPANGO WA RASILIMALIWATU 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Malengo ya Mwongozo 2
1.2.1 Lengo Kuu 2
1.2.2 Malengo Mahsusi 2
1.3 Umuhimu wa Mwongozo 2
1.4 Walengwa wa Mwongozo 2
1.5 Mpangilio wa Mwongozo 2

SURA YA PILI 3
MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIWA KATIKA KUANDAA MPANGO WA RASILIMALIWATU 3
2.1 Utangulizi 3
2.1.1 Uhusiano wa Mpango wa Rasilimaliwatu na Mpango Mkakati 3
2.1.2 Utayari wa Waajiri na Wasimamizi wa Rasilimaliwatu 3
2.1.3 Kutenga Rasilimali Fedha 3
2.1.4 Taarifa Sahihi za Watumishi 3
2.1.5 Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA 3
2.1.6 Nyaraka na Taarifa Muhimu 3
2.1.7 Uelewa wa Watumishi kuhusu Mpango wa Rasilimaliwatu 4

SURA YA TATU 5
HATUA NA MUUNDO WA MPANGO WA RASILIMALIWATU 5
3.1 Hatua Za Kuzingatiwa Katika Maandalizi Ya Mpango Wa Rasilimaliwatu 5
3.1.1 Uchambuzi wa Sera, Malengo, na Mipango ya Taasisi 5
3.1.2 Uchambuzi wa Mazingira ya Utendaji Kazi wa Taasisi 5
3.1.3 Kubaini Mahitaji ya Rasilimaliwatu 6
3.1.4 Kubaini Upatikanaji wa Rasilimaliwatu. 7
3.1.5 Uchambuzi wa Kubaini Upungufu au Ziada ya Rasilimaliwatu. 8
3.1.6 Kuandaa Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu 8
3.1.7 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu 9
3.2 Mbinu za kubaini mahitaji na upatikanaji wa rasilimaliwatu 9
3.2.1 Uzoefu wa Viongozi wa Taasisi. 9
3.2.2 UchambuziwaMwenendowaUwiano (RatioandTrendAnalysis) 9
3.2.3 Mbinu ya Kuchunguza Uzito wa Kazi. 9
3.3 Muundo wa mpango wa rasilimaliwatu 9

SURA YA NNE **11**
MGAWANYO WA MAJUKUMU **11**
4.1 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora 11
4.2 Taasisi za Umma 11
4.3 Kamati ya Mpango wa Rasilimaliwatu katika Taasisi 11
4.4 Wakuu wa Idara na Vitengo 12
4.5 Mkuu wa Idara inayosimamia Rasilimaliwatu 12
4.6 Timu ya Mpango wa Rasilimaliwatu katika Taasisi 12
4.7 Watumishi 12

SURA YA TANO **13**
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA **13**
5.1 Ufuatiliaji na Tathmini 13
5.2 Utoaji Taarifa 13
5.2.1 Umuhimu wa Utoaji Taarifa 13
5.2.2 Aina ya Taarifa zitakazoandaliwa na Taasisi za Umma 13
5.2.3 Uwasilishaji wa Taarifa 14
5.3 Mapitio ya Mpango wa Rasilimaliwatu 14

ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho 1:
Fomu Na. 1: Uchambuzi wa Sera, Malengo na Mipango ya Taasisi 16
Kiambatisho 2:
Fomu Na. 2: Uchambuzi wa Mazingira ya Utendaji Kazi wa Taasisi 18
Kiambatisho 3:
Fomu Na. 3: Kubaini Mahitaji ya Rasilimaliwatu kulingana na Shughuli/ Kazi katika Taasisi 23
Kiambatisho 4:
Fomu Na. 4: Kubaini Mahitaji ya Rasilimaliwatu kulingana na Muundo 25
Kiambatisho 5:
Fomu Na. 5: Uchambuzi wa Rasilimaliwatu iliyopo ndani ya Taasisi katika makundi ya Umri 26
Kiambatisho 6:
Fomu Na. 6: Uchambuzi wa Rasilimaliwatu iliyopo katika Taasisi katika makundi ya Sifa za Kielimu 27
Kiambatisho 7:
Fomu Na. 7: Historia ya Upatikanaji wa Rasilimaliwatu katika Taasisi 28
Kiambatisho 8:
Fomu Na. 8: Kubaini Upatikanaji wa Rasilimaliwatu wa Baadae 29
Kiambatisho 9:
Fomu Na9: Uchambuzi wa Upungufu au Ziada ya Rasilimaliwatu na Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu ya Kuzitatua 30
Kiambatisho 10:
Fomu Na. 10: Kubaini Upatikanaji wa Rasilimaliwatu ya Baadaye 31
Kiambatisho 11:
Fomu Na.11: Mpango Kazi wa Rasilimaliwatu 32
Kiambatisho 12:
Fomu Na. 12: Mpango wa Kuajiri na Uhamisho 33
Kiambatisho 13:
Fomu Na. 13: Mpango wa Upandishwaji Cheo 34
Kiambatisho 14:
Fomu Na. 14: Mpango wa Urithishanaji Madaraka 35
Kiambatisho 15:
Fomu Na. 15: Mpango wa Mafunzo 36
Kiambatisho 16:
Fomu Na.16: Ufatiliaji na tathmini 37
Kiambatisho 17:
Fomu Na. 17: Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu 38

DIBAJI



Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalenga kuimarisha Utumishi wa Umma kwa kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa Rasilimaliwatu ya kutosha inayosimamiwa vizuri ili kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma bora na endelevu kwa wananchi. Katika kufikia lengo hili, Serikali imekuwa ikitekeleza jitihada mbalimbali za kusimamia Rasilimaliwatu. Jitihada hizo ni pamoja na kuandaliwa kwa Kitini cha Mpango wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma cha mwaka 2010 ili kuwezesha Taasisi za Umma kukitumia katika kuandaa na kutekeleza Mpango wa Rasilimaliwatu.

Pamoja na jitihada zilizotekelezwa, kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizoathiri kufikiwa kwa malengo tarajiwa. Changamoto hizo zinajumuisha kutotekelezeka kwa baadhi ya maelekezo yaliyotolewa kutokana na matumizi ya lugha isiyo rafiki katika kitini tajwa; na Taasisi nyingine kuwa na Mipango ya Rasilimaliwatu ambayo haijaandaliwa katika viwango vinavyokubalika kutokana na kukosekana kwa mtiririko wa Mpango katika Kitini hicho.

Katika kutatua changamoto hizo, Serikali imeandaa Mwongozo huu wa Mpango wa Rasilimaliwatu ili kutoa maelekezo mahsusi na rahisi kwa watumiaji kuhusu namna ya kuandaa na kutekeleza Mpango wa Rasilimaliwatu. Mwongozo huu unaainisha hatua zinazopaswa kuzingatiwa katika kubainisha mahitaji ya watumishi; upatikanaji wa idadi stahiki ya watumishi; na Mgawanyo wa Majukumu katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango huo.

Aidha, Mwongozo huu utawezesha Taasisi za Umma kutoa makadirio sahihi ya uhitaji wa Rasilimaliwatu na makisio sahihi ya rasilimali fedha katika maandalizi ya Mishahara na Bajetiya Ikama. Vilevile, Mwongozo huu ni nyenzo itayowezesha uwepo wa watumishi wenye sifa, uwezo na ujuzi stahiki; upangajiwa matumizi sahihi ya Rasilimaliwatu ikiwa ni pamoja na kuwa na Mpango madhubuti wa kuwabakiza watumishi na kuondoa changamoto ya upungufu wa watumishi katika Taasisi pale watumishi wanapoondoka ghafla au kustaafu mapema.

Utekelezaji wa Mwongozo huu, utasaidia katika kuwapata, kuwatumia, kuwaendeleza na kuwabakiza watumishi wenye sifa na uwezo katika Taasisi za Umma na hatimaye kuwezesha Utumishi wa Umma kusimamia rasilimaliwatu ipasavyo ili kufikia malengo na mipango ya kitaifa na kisekta. Hivyo, nawaelekeza waajiri wote katika Utumishi wa Umma kuhakikisha mwongozo huu unatekelezwa kikamilifu na kuongeza tija na ufanisi katika Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma.

Juma S. Mkomi
KATIBU MKUU (UTUMISHI)

FARAHASA

Neno	Tafsiri
Idadi ya watumishi wasiokuwepo kazini	Watumishi ambao hawapo kazini zaidi ya miezi sita kwa sababu mbalimbali kama vile: mafunzo ya muda mrefu, kuugua muda mrefu, likizo bila malipo na sababu nyinginc.
Mpango wa Rasilimaliwatu	Utaratibu mahsusi wa namna ya kuwapata, kuwatumia, kuwaendeleza na kuwabakiza watumishi wenye sifa na uwezo katika Taasisi.
Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu	Mipango midogo midogo ya Kiutumishi ya kuondoa ziada au upungufu wa aina fulani ya watumishi kwa idadi na au sifa. Hii inahusisha Mipango kama kuajiri, mafunzo, uhamisho upandishaji madaraja, urithishanaji madaraka, Taasisi kufanya mpangilio mpya wa Rasilimaliwatu, usimamizi wa utendaji kazi na kubakiza watumishi.
Tange	Orodha ya watumishi kwa kuzingatia ukubwa kazini.
Timu ya Mpango wa Rasilimaliwatu	Watumishi waliochaguliwa kutoka katika Idara zenye watumishi wengi katika Taasisi ili kushirikiana na Idara inayosimamia masuala ya Rasilimaliwatu kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu.

Taasisi za Umma	Ni Taasisi zote zinazojumuisha Taasisi ambazo Serikali ina umiliki wa asilimia 100 ambazo ni Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Wakala za Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma.

SURA YA KWANZA

DHANA YA MWONGOZO WA MPANGO WA RASILIMALIWATU

1.1 UTANGULIZI

Mpango wa Rasilimaliwatu ni mchakato muhimu wa kupata, kutumia, kuendeleza na kubakiza Rasilimaliwatu yenye uwezo na vipaji katika Taasisi. Mchakato huo unawezesha Taasisi kuwa na Rasilimaliwatu ya kutosha, yenye sifa stahiki na tabia sahihi kwa wakati unaotakiwa na pia kupanga rasilimali hiyo mahali sahihi ili kufikia malengo ya Taasisi.

Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma ni rasilimali muhimu na yenye thamani ambayo inahitaji kusimamiwa ipasavyo ili kuleta ufanisi na tija katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Kwa kuzingatia umuhimu huo, mwaka 2010 Serikali kupitia Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma iliandaa Kitini cha Mpango wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma. Kitini hicho kililenga kuziwezesha Taasisi za Umma kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Serikali na kuitekeleza Mipango hiyo kikamilifu ili kuimarisha uwezo wa Rasilimaliwatu katika kutoa huduma kwa weledi na maarifa.

Hata hivyo, kumekuwa na changamoto za utekelezaji wa Kitini hicho kwa baadhi ya Taasisi za Umma kushindwa kukitumia ipasavyo kutokana matumizi ya lugha isiyo rafiki; na Taasisi nyingine kuwa na Mipango ya Rasilimaliwatu ambayo haijaandaliwa katika viwango vinavyokubalika kutokana na kukosekana kwa mtiririko wa Mpango.

Hali hii imeathiri usimamizi wa Rasilimaliwatu na kusababisha kuwepo kwa ziada au upungufu wa watumishi uliopelekea kushuka kwa morali ya kazi, utendaji kazi hafifu, baadhi ya watumishi kutopata fursa za kuendelezwa kupitia mipango mahsusi ya Rasilimaliwatu ikiwemo Mpango wa Mafunzo, Mpango wa Motisha na Mpango wa Urithishanaji Madaraka.

Katika kukabiliana na changamoto zilizobainishwa na kwa kuzingatia maelekezo ya kifungu 35A (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 na Kanuni 102 (3) za Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, Serikali imeandaa Mwongozo huu wa Kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu ambao ni rahisi kutumika katika kuandaa na kutekeleza Mpango wa Rasilimaliwatu.

Mpango wa Rasilimaliwatu ni nyenzo ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu inayotekelezwa kama sehemu muhimu ya Mpango Mkakati wa Taasisi na Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Fedha. Mahitaji yanayoainishwa katika Ikama na Bajeti ya Mishahara yanatakiwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa katika Mpango wa Rasilimaliwatu wa Taasisi.

1.2 MALENGO YA MWONGOZO

1.2.1 Lengo Kuu

Kuweka utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa na Waajiri na Wasimamizi wa Rasilimaliwatu katika Taasisi za Umma wakati wa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Rasilimaliwatu.

1.2.2 Malengo Mahsusi

i. Kuwezesha Taasisi za Umma kuweza kubaini mahitaji ya Rasilimaliwatu yenye sifa, uwezo na tabia stahiki kwa wakati husika;
ii. Kuweka utaratibu wa kuzingatiwa katika kubainisha mahitaji ya watumishi;
iii. Kuelekeza Taasisi za Umma namna ya kuwa na kutumia rasilimaliwatu inayohitajika kulingana na mgawanyo wa majukumu wa Taasisi; na
iv. Kuweka utaratibu sahihi wa utoaji wa taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu kwa maamuzi mbalimbali.

Kupitia utekelezaji wa malengo haya, Taasisi za Umma zitaweza kuchambua na kubaini mahitaji halisi ya Rasilimaliwatu, upatikanaji wake na kuainisha Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu, fursa zinazojitokeza pamoja na kukabiliana na changamoto za kiutumishi, mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kidemografia na kiteknolojia

1.3 UMUHIMU WA MWONGOZO

Mwongozo huu unaweka utaratibu wa kuzingatiwa katika kuimarisha mifumo ya usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Taasisi za Umma. Utekelezaji wa Mwongozo utaziwezesha Taasisi za Umma na Sekta ya Utumishi wa Umma kwa ujumla katika masuala yafuatayo:-

i. Kuimarisha mbinu za kubaini mahitaji na upatikanaji wa Rasilimaliwatu kwa wakati wa sasa na baadae;
ii. Kupanga matumizi sahihi ya Rasilimaliwatu;
iii. Kubaini changamoto za Rasilimaliwatu zinazotokana na maradhi, ushindani katika soko la ajira, upungufu wa sifa, uwezo, ujuzi, ukomo wa utumishi na kuchukua hatua stahiki;
iv. Kuwa na makadirio sahihi ya mahitaji halisi katika maandalizi ya bajeti ya Ikama na Mishahara; na
v. Kuimarika kwa mbinu za usimamizi wa Rasilimaliwatu na ufanyaji maamuzi sahihi ya kiutumishi.

1.4 WALENGWA WA MWONGOZO

Mwongozo huu umelenga kutumiwa na Wasimamizi wa Rasilimaliwatu katika Taasisi zote za Umma zikiwemo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Wakala za Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma.

1.5 MPANGILIO WA MWONGOZO

Mwongozo huu unajumuisha Sura Tano (5). Sura ya Kwanza inatoa maelezo ya Utangulizi na Malengo ya Mwongozo; Sura ya Pili inabainisha Masuala Muhimu ya Kuzingatiwa katika Kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu; Sura ya Tatu inaonesha Hatua na Muundo wa Mpango wa Rasilimaliwatu; Sura ya Nne inatoa Mgawanyo wa Majukumu; na Sura ya Tano inabainisha Mikakati ya Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa. Mwongozo pia unajumuisha orodha ya Viambatisho vinavyotoa maelezo ya kina katika maeneo mbalimbali ya Mwongozo.

SURA YA PILI

MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIWA KATIKA KUANDAA MPANGO WA RASILIMALIWATU

2.1 UTANGULIZI

Maandalizi ya Mpango wa Rasilimaliwatu yatazingatia masuala mbalimbali ya msingi katika Utumishi wa Umma. Masuala hayo ni:-

2.1.1 Uhusiano wa Mpango wa Rasilimaliwatu na Mpango Mkakati

Mpango wa Rasilimaliwatu uandaliwe kama sehemu muhimu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi kwa kuainisha mahitaji ya Rasilimaliwatu kwa idadi, sifa, uwezo, ujuzi na tabia sahihi ili kufikia malengo ya Mpango Mkakati. Timu inayoandaa Mpango wa Rasilimaliwatu iwe na uelewa na izingatie Dira, Dhima na Malengo ya kimkakati pamoja na Miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Taasisi.

2.1.2 Utayari wa Waajiri na Wasimamizi wa Rasilimaliwatu

Waajiri na wasimamizi wa Rasilimaliwatu kutambua Rasilimaliwatu kama nyenzo muhimu kwa ufanisi wa Taasisi na kuwa na utayari wa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Rasilimaliwatu kama inavyopaswa. Wakuu wa Idara na Vitengo wahusishwe katika mchakato mzima wa kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu kwa kuwa wanasimamia watumishi na wanatambua mahitaji ya Rasilimaliwatu ili kutekeleza kazi wanazosimamia.

2.1.3 Kutenga Rasilimali Fedha

Taasisi zitenge rasilimali fedha kwenye bajeti zake kwa ajili ya kuandaa au kuhuisha, kutekeleza, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu.

2.1.4 Taarifa Sahihi za Watumishi

Taasisi zihakikishe zinatumia taarifa sahihi katika maandalizi ya Mpango wa Rasilimaliwatu ili kuwezesha kufanya uamuzi sahihi na wenye manufaa. Aidha, uchambuzi wa taarifa hizo uzingatie masuala ya Anuai za Jamii kama vile jinsia na ulemavu ili yajumuishwe kikamilifu katika maandaalizi ya Mpango wa Rasilimaliwatu.

2.1.5 Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA

Utekelezaji wa Mwongozo huu uzingatie fursa za mifumo ya TEHAMA ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu inayotumika katika Utumishi wa Umma.

2.1.6 Nyaraka na Taarifa Muhimu

Nyaraka zifuatazo zitapaswa kuzingatiwa wakati wa kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu:-

i. Muundo na Mgawanyo wa Majukumu wa Taasisi;
ii. Mpango Mkakati wa Taasisi;
iii. Miundo ya Maendeleo ya Utumishi;
iv. Orodha ya Ukubwa Kazini (Tange);

v. Maelezo ya kazi ya kila nafasi;
vi. Orodha ya kazi;
vii. Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mipango mingine maalum ya Taasisi, Sekta au Taifa yenye mahitaji maalum ya Rasilimaliwatu;
viii. Taarifa kuhusu mwenendo wa soko la ajira kitaifa, kikanda na kimataifa iliyoandaliwa na Wizara yenye dhamana ya masuala ya Kazi na Ajira, Taasisi za Elimu ya Juu na Mamlaka za Usimamizi wa Kitaaluma; na
ix. Taarifa na Nyaraka nyingine muhimu zinazohusu Rasilimaliwatu.

2.1.7 Uelewa wa Watumishi kuhusu Mpango wa Rasilimaliwatu

Taasisi itapaswa kujenga uelewa wa watumishi kuhusu Mpango wa Rasilimaliwatu ulioandaliwa kabla ya kuidhinishwa na Mamlaka husika kwa ajili ya kupata/ kujenga umiliki (ownership).

SURA YA TATU

HATUA NA MUUNDO WA MPANGO WA RASILIMALIWATU

3.1 HATUA ZA KUZINGATIWA KATIKA KUANDAA MPANGO WA RASILIMALIWATU

Maandalizi ya Mpango wa Rasilimaliwatu yanajumuisha hatua kuu saba (7) zinazopaswa kuzingatiwa katika mtiririko ufuatao:-

3.1.1 Uchambuzi wa Sera, Malengo, na Mipango ya Taasisi

Hatua hii inahusisha kuchambua Dira, Dhima, Mpango Mkakati, Sera, Programu zilizopangwa na miradi iliyopo ili kubaini mahitaji ya Rasilimaliwatu kwa idadi na sifa (maarifa, ujuzi na tabia) itakayowezesha kufikiwa kwa Malengo ya Taasisi. Aidha, mahitaji ya watumishi wa mikataba yakibainika nayo yajumuishwe katika Mpango wa Rasilimaliwatu **(Kiambatisho Na. 1 ni Fomu itakayotumika).**

Katika Uchambuzi wa Malengo, Sera na Mipango ya Taasisi, masuala yafuatayo yazingatiwe: -

i. Dira, Dhima, Majukumu na Malengo ya Taasisi kulingana na Mpango Mkakati wa Taasisi ili kuweka mipango ya rasilimaliwatu itakayowezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa;
ii. Sera, Mipango, Programu mbalimbali zilizopo katika Taasisi ili kubaini masuala yenye mtazamo chanya au hasi yanayoathiri Mpango wa Rasilimaliwatu; na
iii. Uchambuzi wa Muundo na Mgawanyo wa majukumu wa Taasisi uwezeshe kutambua nafasi zilizopo za uongozi, mgawanyo wa kazi, uratibu na usimamizi wa Rasilimaliwatu.

3.1.2 Uchambuzi wa Mazingira ya Utendaji Kazi wa Taasisi

Hatua hii inahusisha uchambuzi wa mazingira ya utendaji kazi ya ndani na nje ya Taasisi ambayo yanaweza kuleta athari hasi au chanya katika utendaji kazi wa watumishi na Taasisi. Uchambuzi wa Mazingira ya Nje ya Taasisi unahusisha kutambua mambo yaliyopo nje ya Taasisi ambayo yanaweza kuathiri Rasilimaliwatu iliyopo katika Taasisi kisiasa, kiuchumi, kijamii, kisheria, kiteknolojia na kidemografia. Uchambuzi wa Mazingira ya Ndani ya Taasisi unahusisha uchambuzi wa Mpango Mkakati, Sera, Kanuni, mifumo ya kiutumishi, mazingira ya kazi, afya na mahusiano ya watumishi na mipango mingine ya Taasisi. Uchambuzi wa mazingira ya ndani na ya nje ya Taasisi hutoa taarifa juu ya upungufu na au ziada ya watumishi kwa idadi na au sifa katika kutekeleza kazi za Taasisi **(Kiambatisho Na.2 ni Fomu itakayotumika)**.

Katika kufanya uchambuzi wa mazingira ya utendaji kazi ya ndani na ya nje ya Taasisi, yafuatayo yazingatiwe:-

i. Kuchambua mifumo ya kiutumishi ya ndani, Sera na mazingira ya kazi ambayo yanaathiri hali ya Rasilimaliwatu ya sasa na baadae katika Taasisi; na
ii. Kuchambua mazingira ya nje ya Taasisi ambayo yanaathiri Rasilimaliwatu ya sasa na ya baadae ya Taasisi.

Mfano wa mitazamo chanya au hasi inayoathiri Mpango wa Rasilimaliwatu kuendana na Mazingira Kubaini Mahitaji ya Rasilimaliwatu

Kutokana na ukuaji wa Teknolojia, Wizara ya Maji imeweza kuboresha huduma zake. Kwa mfano, wateja wanatumiwa ankara za huduma za maji na kulipa kwa njia ya kielektroniki badala ya mfumo wa zamani wa kutumiwa ankara za maji kwa njia ya posta na wateja kwenda kwenye ofisi zao kulipa ankara hizo.

Athari ya teknolojia katika mtazamo chanya au hasi wa Mpango wa Rasilimaliwatu ni kama ifuatavyo:

Mtazamo Chanya

i. Kufundisha watumishi juu ya ujuzi na uelewa wa TEHAMA ili kuweza kusimamia mfumo wa malipo ya kielektroniki kwa ufanisi na kuongeza makusanyo ya Taasisi;
ii. Idara kuwa na vifaa vya kielektroniki na vifaa vingine kwa ajili ya matumizi ya ofisi; na
iii. Kuendeleza miundombinu ya TEHAMA katika matawi yote ili kuwawezesha wateja kuunganishwa na huduma ya maji.

Mtazamo Hasi

Kupunguza au kuwabadilishia kazi watumishi waliokuwa wakifanya kazi ya kusambaza ankara; na Ongezeko la gharama za mafunzo zinazotokana na kuwabadilishia kazi watumishi na kutoa elimu kwa wateja.

3.1.3 Kubaini Mahitaji ya Rasilimaliwatu

Hatua hii inahusisha kubaini mahitaji ya Rasilimaliwatu ambayo ni muhimu kwa Taasisi katika kutekeleza malengo na mipango yake. Uchambuzi ufanyike kwa kuangalia majukumu yanayotekelezwa kwa sasa na baadae, uzito wa kazi, idadi na sifa za watumishi zinazohitajika kwa kuzingatia mwenendo wa kimataifa, kikanda na kitaifa unaoweza kuathiri mahitaji ya Rasilimaliwatu ya Taasisi.

Ili kubaini mahitaji ya Rasilimaliwatu ya baadae ya Taasisi njia zifuatazo zitumike:-

i. Uchambuzi wa Rasilimaliwatu: Njia hii inahusisha uchambuzi wa Rasilimaliwatu waliopo ikilinganishwa na majukumu ya Taasisi ili kubaini mahitaji ya baadae ya idadi na sifa za watumishi wanaohitajika; na
ii. Uchambuzi wa uzito wa kazi: Njia hii inahusisha kuchambua aina ya kazi zinazofanywa sasa na zile zitakazofanyika baadae na kubaini mahitaji ya Rasilimaliwatu kwa idadi, sifa na ujuzi unaotakiwa kufanya kazi hizo **(Kiambatisho Na. 3 na 4 ni fomu zitakazotumika)**.

Katika kubaini mahitaji ya Rasilimaliwatu mambo yafuatayo yazingatiwe:-

a. Kuchambua Muundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Taasisi uliopo sambamba na malengo yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati;
b. Kuzingatia utekelezaji wa mipango ya sasa na baadae kwa kila Idara na Kitengo katika kutambua Rasilimaliwatu inayohitajika kwa idadi, sifa, mgawanyo wa kazi na mahali watakapofanyia kazi;
c. Kuchambua orodha za kazi na maelezo ya kazi ili kubainisha shughuli zinazotekelezwa na mahitaji ya Rasilimaliwatu ya baadae; na

d. Kuchambua majukumu ya sasa na baadae, nafasi na kazi zitakazohitajika ili kutambua mahitaji ya rasilimaiwatu kiidadi, kisifa na ujuzi.

Aidha, taarifa zinazotokana na Mfumo wa kubaini mahitaji ya Rasilimaliwatu (e-Msawazo) zitumike katika kukamilisha hatua hii.

3.1.4 Kubaini Upatikanaji wa Rasilimaliwatu

Hatua hii inahusisha uchambuzi wa Rasilimaliwatu iliyopo na upatikanaji wake wa baadae. Hatua hii ifanyike kwa kuangalia watumishi waliopo ndani ya Taasisi. Ikibainika kuwa wapo watumishi wa ziada katika Idara au Kitengo, ziada hiyo inaweza kutumika kama njia ya upatikanaji wa Rasilimaliwatu katika Idara nyingine ndani ya taasisi husika au kwenda nje kwa ajili kutumika katika Taasisi nyingine za Umma. Ikiwa Rasilimaliwatu ya ndani haikidhi mahitaji yaliyobainishwa, Taasisi iangalie upatikanaji wa Rasilimaliwatu kutoka katika Taasisi nyingine za Umma au katika soko la ajira **(Kiambatisho 5 hadi 8 ni Fomu zitakazotumika).**

Katika kubaini upatikanaji wa Rasilimaliwatu yafuatayo yazingatiwe: -

i. Kuwashirikisha Wakuu wa Idara na Vitengo ili kupata idadi ya watumishi kwa idadi, sifa, ujuzi, umri, jinsi, nafasi na aina za kazi wanazofanya sasa na watakazofanya baadae; na

ii. Kubaini idadi ya Rasilimaliwatu itakayopatikana baada ya kuzingatia mwenendo wa watumishi kutoka katika Idara au Kitengo kimoja kwenda kingine; walivyotoka nje ya Taasisi kuingia ndani (inaongeza idadi ya Rasilimaliwatu) na watumishi waliotoka ndani kwenda nje ya Taasisi (inapunguza idadi ya Rasilimaliwatu).

Hivyo, yafuatayo yafanyike:-

a. Kukadiria idadi ya watumishi wanaoingia ndani ya Taasisi kwa upandishwaji vyeo, uhamisho, kuazimwa, kurejea katika ajira, ajira mpya na kumbadilishia kazi mtumishi kutoka nje ya Taasisi;

b. Makadirio ya idadi ya watumishi wanaoweza kuondoka kwa kustaafu, kuazimwa, kuacha kazi, vifo na sababu nyingine ambazo ni vigumu kuzibashiri lakini inawezekana kuzikadiria kwa kuangalia taarifa za nyuma zinazuonesha mienendo ya watumishi; na

c. Kubaini watumishi wa Taasisi ambao hawapo kwa kipindi cha miezi sita (6) au zaidi kutokana na ugonjwa, kuazimwa na Taasisi nyingine na likizo bila malipo. Sababu hizi zizingatiwe katika kubaini watumishi wanaohitajika kwa kuwa majukumu yao lazima yatekelezwe wakati hawapo. Hivyo, idadi hiyo ya watumishi ambao hawapo itambuliwe katika idadi kamili ya watumishi wa Taasisi.

iii. Kuchambua kwa kina matumizi ya Rasilimaliwatu iliyopo ili kubaini kama kuna watumishi katika baadhi ya Idara au Vitengo wanatumika chini ya kiwango au kuna ziada ya watumishi kwa kulinganisha na huduma inayotakiwa kutolewa;

iv. Kuzingatia kuhama kwa watumishi ndani ya Taasisi kutokana na matokeo ya kupandishwa vyeo, kubadilishwa kazi na kupangiwa kazi mpya.
Hali hii haina athari katika jumla kuu ya watumishi waliopo sasa na baadaye katika ngazi ya Taasisi lakini inaweza kuonesha kushuka au kupanda kwa idadi ya watumishi katika ngazi ya Idara au Vitengo vya Taasisi; na

v. Kukokotoa idadi ya watumishi watakaokuwepo katika Taasisi hapo baadae kwa wakati husika.

Kielelezo Na. 1 kinaonesha jinsi ya kukokotoa.



Kielelezo Na.1: Kikokotoo cha Idadi ya Watumishi wanaotakiwa kuwepo

3.1.5 Uchambuzi wa Kubaini Upungufu au Ziada ya Rasilimaliwatu

Hatua hii inatokana na matokeo ya hatua ya tatu na ya nne ambapo inabaini upungufu na au ziada ya Rasilimaliwatu ambayo inahitaji kujazwa au kuondolewa na Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu. Upungufu unaweza kuwa katika idadi (kiasi) au sifa (ubora) au zote mbili kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadae ya Rasilimaliwatu. Katika kufanya uchambuzi wa upungufu au ziada, yafuatayo yafanyike:-

i. Kutambua uhaba/upungufu wa Rasilimaliwatu kwa sasa na baadae, kwa idadi, sifa na uwezo katika Kada tofauti za watumishi na usawa wa kijinsia. Upungufu hutokea wakati mahitaji ya Rasilimaliwatu yanapozidi upatikanaji.
ii. Kutambua ziada ya watumishi katika nafasi na Kada mbalimbali kwa idadi na sifa. Hali hii yaweza kutokea kutokana na watumishi kupangwa sehemu ambazo hawahitajiki. Ziada ya watumishi hutokea pale ambapo upatikanaji wa Rasilimaliwatu ni zaidi ya mahitaji; na
iii. Pale ambapo mahitaji ya Rasilimaliwatu ni sawa na upatikanaji, hakuna hatua yoyote inayotakiwa kuchukuliwa. Hali hii ni nadra kutokea, inamaanisha kuwa Taasisi imejipanga vizuri, ina mipango mizuri na haina mahitaji ya Rasilimaliwatu kwa wakati huo. **(Kiambatisho Na. 9 kinaonesha mifano ya upungufu na ziada ya Rasilimaliwatu na hatua za kuchukua wakati Kiambatisho Na. 10 kinaonesha fomu itakayotumika)**

3.1.6 Kuandaa Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu

Baada ya kubaini upungufu au ziada ya Rasilimaliwatu kwa idadi au sifa, hatua inayofuata ni kuainisha Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu ili kuondoa upungufu au ziada ya Rasilimaliwatu iliyobainika. Katika kuainisha Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu, yafuatayo yafanyike:-

i. Kuondoa upungufu wa watumishi kiidadi na/au kisifa kwa kuhusisha Mipango kama vile kuajiri, uhamisho wa ndani au wa nje, upandishaji madaraja, mafunzo, urithishanaji madaraka, Taasisi kufanya mpangilio mpya wa Rasilimaliwatu, usimamizi wa utendaji kazi na Mpango wa kubakiza watumishi; na
ii. Kuondoa ziada ya watumishi kwa kuwabadilishia kazi, kupunguza watumishi, kuwapangia kazi nyingine au kuwahamishia Idara/Kitengo kingine au Taasisi nyingine.

Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu iandaliwe Mpango Kazi na itengewe bajeti kwa ajili ya utekelezaji. Aidha, utekelezaji wa Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu ufanyike kwa kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano. **(Kiambatisho 11-15 ni fomu zitakazotumika)**.



Kielelezo Na. 2 Muundo wa Mpango wa Rasilimaliwatu

SURA YA NNE

MGAWANYO WA MAJUKUMU

4.1 OFISI YENYE DHAMANA YA USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu katika Taasisi zote za Umma;
ii. Kutoa usaidizi na ushauri wa kitaalamu katika hatua za uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu;
iii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu; na
iv. Kufanya mapitio ya Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu pale inapohitajika.

4.2 TAASISI ZA UMMA

i. Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Rasilimaliwatu wa Taasisi husika kwa mujibu wa Mwongozo;
ii. Kuhakikisha mipango mahususi iliyobainishwa katika Mpango wa Rasilimaliwatu wa Taasisi inajumuishwa katika bajeti na mipango kazi ya mwaka ya Taasisi;
iii. Kuunda Kamati ya kusimamia shughuli za Mpango wa Rasilimaliwatu;
iv. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu katika ngazi ya Taasisi;
v. Kuandaa taarifa za kila nusu za utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu na kuziwasilisha katika Menejimenti ya Taasisi husika; na
vi. Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu katika Ofisi yenye dhamana na usimamizi wa Utumishi wa Umma.

4.3 KAMATI YA MPANGO WA RASILIMALIWATU KATIKA TAASISI

Katika usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu, Mkuu wa Taasisi atateua Kamati ambayo itakuwa na jukumu la msingi la kuhakikisha Mpango wa Rasilimaliwatu umeandaliwa kama sehemu muhimu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi.

a. Wajumbe wa Kamati

Muundo wa Wajumbe wa Kamati hii watakuwa ni kama ifuatavyo:-

i. Mkuu wa Idara au Kitengo kinachohusika na Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
ii. Mkuu wa Idara au Kitengo kinachoshughulikia Sera na au Mipango;
iii. Mkuu wa Idara ya Uhasibu na Fedha;
iv. Mwakilishi wa Chama cha Wafanyakazi mahala pa kazi chenye uwakilishi mkubwa;
v. Wajumbe wengine kutoka Idara za msingi za Taasisi; na
vi. Mkuu wa Sehemu inayohusika na Usimamizi wa Rasilimaliwatu au Afisa Utumishi kuanzia ngazi ya Afisa Mwandamizi atakuwa Katibu wa Kamati.

b. Majukumu ya Kamati

i. Kuhakikisha masuala ya Rasilimaliwatu yamezingatiwa katika Idara au Vitengo ili kufikia Malengo ya Taasisi;

ii. Kuhakikisha Mipango Mahsusi ya utendaji kazi ya Rasilimaliwatu imeainishwa na kujumuishwa katika Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Fedha;
iii. Kujadili changamoto zinazotokana na utekelezaji wa Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu na athari zinazoweza kujitokeza katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu;
iv. Kupitia na kuwasilisha Rasimu ya Mpango wa Rasilimaliwatu kwenye Menejimenti kwa ajili ya kuidhinishwa; na
v. Kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu na kuiwasilisha kwenye Menejimenti.

4.4 WAKUU WA IDARA NA VITENGO

i. Kutoa taarifa muhimu za Rasilimaliwatu wakati wa maandalizi ya Mpango;
ii. Kupanga watumishi kulingana na Mpango wa Rasilimaliwatu ulioidhinishwa;
iii. Kuangalia mwenendo na kupima utendaji kazi wa watumishi;
iv. Kufanya tathmini ya mahitaji ya ujuzi ya watumishi ili kubaini mafunzo yanayohitajika; na
v. Kutoa mafunzo na fursa za kuwaendeleza watumishi.

4.5 MKUU WA IDARA INAYOSIMAMIA RASILIMALIWATU

i. Kuratibu shughuli zote za Kamati ya Mpango wa Rasilimaliwatu;
ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu;
iii. Kukusanya taarifa muhimu za Rasilimaliwatu kwa idadi na sifa kutoka kila Idara na Vitengo;
iv. Kuhuisha takwimu za Rasilimaliwatu kwa ajili ya maandalizi ya Mpango wa Rasilimaliwatu;
v. Kuteua watumishi watakaounda Timu itakayoandaa Mpango wa Rasilimaliwatu kwa kushauriana na Wakuu wa Idara na Vitengo;
vi. Kuwasilisha Rasimu ya Mpango wa Rasilimaliwatu kwenye Kamati ya Mpango wa Rasilimaliwatu;
vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu;
viii. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Mpango wa Rasilimaliwatu; na
ix. Kuandaa Ikama na Bajeti ya Mishahara kwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa katika Mpango wa Rasilimaliwatu.

4.6 TIMU YA MPANGO WA RASILIMALIWATU KATIKA TAASISI

Timu ya Mpango wa Rasilimaliwatu itateuliwa na Mkuu wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu. Wajumbe wa Timu watakuwa ni watumishi kutoka Idara/ Kitengo au Sehemu ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu na watumishi wawakilishi kutoka katika Idara za msingi na baadhi ya Vitengo vilivyopo kwenye Taasisi husika. Majukumu ya Timu yatakuwa ni pamoja na:-

i. Kukusanya takwimu za Rasilimaliwatu kutoka kwenye Idara na Vitengo kwa ajili ya maandalizi ya Mpango wa Rasilimaliwatu;
ii. Kuchambua mahitaji, upungufu au ziada, na upatikanaji wa Rasilimaliwatu kutokana na taarifa za kiutumishi za Idara na Vitengo na kwa kuzingatia Nyaraka na Taarifa Muhimu zilizoainishwa Sehemu ya 2.1.6 ya Mwongozo huu;
iii. Kuainisha Mipango Mahsusi ya Rasilimaliwatu na kuandaa Mpango Kazi; na
iv. Kuandaa Rasimu ya Mpango wa Rasilimaliwatu na kuiwasilisha kwa Mkuu wa Idara inayohusika na Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu.

4.7 WATUMISHI

i. Kutekeleza majukumu waliyopangiwa katika Taasisi;
ii. Kutoa mapendekezo ya maeneo ya **kuendelezwa** wakati wa tathmini ya utendaji kazi na zoezi la tathmini ya mahitaji ya mafunzo; na
iii. Kuwa tayari kujiendeleza kitaaluma.

SURA YA TANO

UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

5.1 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Taasisi za Umma zitakuwa na jukumu la kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu ili kubainisha mafanikio ya utekelezaji, changamoto na upungufu uliopo na kutoa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hizo. Taasisi zitatakiwa kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini (Monitoring and Evaluation Plan) wenye viashiria vya matokeo ya malengo yaliyobainishwa katika Mpango wa Rasilimaliwatu wa Taasisi. Vilevile, Taasisi zote zitatakiwa kutenga bajeti ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa afua za Mpango. Aidha, ufuatiliaji utafanyika katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu.

Kutakuwa na tathmini mbili za utekelezaji wa Mpango ambazo zitahusisha Tathmini ya Muda wa Kati (Mid-term evaluation) ambayo itafanyika baada ya miaka miwili na nusu (2.5) na Tathmini ya Mwisho (End-term Evaluation) itafanyika mwaka wa tano (5). Ufuatiliaji na tathmini utafanikisha upatikanaji wa taarifa muhimu zitakazowezesha kufanya mapitio ya Mpango wa Rasilimaliwatu.

5.2 UTOAJI TAARIFA

5.2.1 Umuhimu wa Utoaji Taarifa

Taarifa za utekelezaji wa Mpango ni muhimu katika kuziwezesha Mamlaka kufanya maamuzi sahihi ambayo yatawezesha Utumishi wa Umma kuwa na Rasilimaliwatu ya kutosha na inayotumika ipasavyo na hivyo kufanya kazi kwa ufanisi. Taasisi za Umma zitatakiwa kutoa taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu kwa kuzingatia taratibu za Serikali za utoaji wa taarifa. Taarifa zitaonesha hali halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu uliofanyika katika Taasisi husika.

5.2.2 Aina ya Taarifa zitakazoandaliwa na Taasisi za Umma

